inaelezwa kuwa na kuficha mambo. Hii ina maana kuwa, riwaya ina mambo mengi ambayo hayaelezwi waziwazi, yanayotokana na uajinabishaji na usahilishaji wa mbinu zake za kisanaa. Mbinu ya uajinabishaji inaelezwa kuwa, ni namna riwaya zinavyojikita katika kusawiri masuala ya kijamii na utamaduni kwa kutumia mtindo mpya. Kwa maana kuwa mwanadamu anaweza kurejeshwa katika muktadha fulani wa jamii yake katika mtindo usioweza kufikiriwa wala kudhaniwa kamwe. Ama, mbinu ya usahilishaji wa masuala ya kijamii inajitokeza kutokana na namna watunzi wanavyoeleza masuala mazito katika jamii ambayo yasiyowezekana katika ulimwengu halisi na kufanya yawezekane na kutekelezeka. Sifa ya mwandishi kuficha mawazo yake katika riwaya ya Kiswahili yalishika nguvu na kuwa mtindo maalum baada ya riwaya hiyo kupiga hatua ya maendeleo katika ubunifu wake. Maendeleo hayo, yanatokana na umahiri wa kutumia mbinu ya uajinabishaji na kuweza kuunda wahusika ambao wanaonekana na upya katika jamii halisi. Pia, wahusika hao wamesawiriwa kwa mbinu ya usahilishaji kwa namna walivyobebeshwa ujumbe mzito kupitia lugha inayoonekana kuwa ya kawaida. Hali hiyo imeijenga riwaya na kuonekana kuwa na sifa ya kuficha maana. Kwa jumla, uajinabishaji na usahilishaji ni mbinu zinazojenga umajaribio katika riwaya. Umajaribio huo unatokana na kupinga kaida zilizozoeleka katika uandishi wa riwaya hasa kanuni za kimagharibi kurudi katika mtindo wa kifasihi simulizi (Senkoro, 2011 na Samwel, 2015). Mbatiah (2019) anasema kuwa, umajaribio unajenga ugumu katika riwaya, ila Samwel (2015) anasisitiza kuwa, ugumu wake haupo katika mtindo wa kifasihi simulizi tu, bali hata katika matumizi ya mtindo wa kisayansi unaobeba masuala ya kifalsafa na kisaikolojia ndani yake. Kwa jumla, riwaya za kimajaribio zimekuwa na mbinu za kisanaa zilizojengwa kwa umahiri mkubwa kiasi ya kujenga maana fiche ndani yake.

Hata hivyo, Mbatiah (1998) na Jilala (2016) wanaona kuwa, riwaya ya majaribio kupitia mtindo wake wa maana fiche kunaitia fasihi ya Kiswahili katika fasihi ya uduni. Pia, wanaiona kuwa, fasihi ya aina hii haielekei kuwa na umuhimu mkubwa katika mazingira ya Afrika ya Mashariki ila kukwamisha uandishi badala ya kuuendeleza. Hoja ya msingi wanayoisimamia ni kuona kuwa, kazi hizi zinakwamisha mawasiliano baina ya fanani na hadhira yake. Ndio maana Mwamzandi (2013) anaeleza kuwa, riwaya ya kimajaribio inaitenga sehemu ya hadhira kwa kumkumbatia msomaji aliyesoma na kuzamia fani adimu za kijamii, kama vile falsafa, saikolojia na sayansi kwa jumla. Imezoeleka kuwa, riwaya ni kazi inayotungwa kwa lugha rahisi na iliyonyooka katika kuwasilisha ujumbe wake. Hivyo, kutumia taswira na picha zisizowazi ni kuichanganya hadhira ya kazi hizo. Maelezo haya yanathibitishwa na Mbatiah (2019) kwa kusema kuwa, riwaya ya majaribio huwasilisha ujumbe wake kwa kutumia taashira, sitiari, visasili na mdokezo badala ya maelezo ya ufafanuzi. Mambo hayo yanamfanya msomaji asipate mawazo yaliyokusudiwa kwa njia iliyowazi. Kwa jumla, riwaya ya majaribio inatumia mtindo wa maana fiche, mtindo ambao unaonekana haumsaidii hadhira wa kawaida kupata ujumbe wa kazi hiyo wala hauisadii tasnia ya riwaya kukua na kuendelea kifasihi. Mtazamo ambao unapingwa na baadhi ya wachambuzi wa riwaya ya kimajaribio wenye mtazamo chanya juu ya mtindo wa maana fiche.

Kinachobainika ni kuwa, riwaya ya kimajaribio ni riwaya iliyokuja kujenga hadhi ya riwaya ya Kiswahili kitaifa na kimataifa. Fani na maudhui ya riwaya hii imekuwa ikivuka mipaka ya jamii ya Afrika ya Mashariki na kuingia katika fasihi ya kilimwengu. Maelezo haya yanathibitishwa na Mkufya (2005) kwa kusema kuwa, riwaya ya kimajaribio si ya Waafrika peke yao. Mkufya anaendelea kusema kuwa, wanaotetea fasihi ya Uafrika, hawajui kwa sababu wameshatenganishwa na Uafrika wao halisi kwa muda mrefu. Riwaya ya *Nagona* imekuwa ikijadili masuali nyeti ambayo hayawezi kujadiliwa waziwazi kutokana na unyeti wao. Kama ambavyo Khamis (2005) anasema kuwa, kazi hizo ni za kisaikolojia zinazojikita na ukweli wa anguko la mifumo ya kidini, kisiasa, kiuchumi na kiutamaduni. Ndio maana Khamis (2007a) anasema, riwaya hii imeibuka kuja kuvunja minyororo ya waandishi wa kuitikia hewalla kwa kila jambo kwa kutumia vipengele mbalimbali vya kisanaa ambavyo vitawaweka salama dhidi ya wenye mamlaka na nguvu ya utawala. Kwa maana, mtindo wa kutumia maana fiche umekuwa ni mtindo unaompa uhuru mwandishi kusema anachokitaka bila ya kudhibitiwa na chambo cha aina yoyote. Pia, ni kazi inayompa hadhira undani wa mambo katika jamii kwa kina sana, kwa sababu mwandishi anakuwa huru kuichambua jamii katika hali tofauti. Ponera na Mkomwa (2019) wanathibitisha hoja hiyo kwa kusema, waandishi wa kimajaribio hutumia riwaya kama chombo cha kutolea falsafa zao zinazotokana na tajiraba ya maisha ya jamii zao na ulimwengu kwa jumla. Tajiriba ambazo huwapa fursa ya kutumia jazanda zinazojenga ugumu wa kazi hizo, kutokana na jazanda hizo kuwa mbali na tajiriba, mantiki na matarajio ya wasomaji wake. Miongoni mwa kipengele cha msingi katika ujenzi wa maana fiche katika riwaya hiz ni kipegele cha wahusika.

**1.3 Wahusika katika Ujenzi wa Maana Fiche**

Wahusika ni kipengele muhimu sana kinachopatikana katika kazi za fasihi ikiwemo riwaya. Riwaya hizo hutumia wahusika kuwasilisha ujumbe wenye maana mbalimbali kwa hadhira lengwa. Maelezo haya yanathibitishwa na Pembe (2017) kwa kusema kuwa, waandishi huteua majina ya wahusika wao na kuyafungamanisha na matukio kwa lengo la kudokeza maana kwa hadhira. Uteuzi huo hudokeza mtazamo wa kiimani, kikazi, kielimu, kikabila na kitabia. Ndio maana inasemwa kuwa, wahusika hutumika kudokeza falsafa ya mwandishi na hata jamii nzima katika kazi husika, (Kawira na Kisurulia, 2017). Ila matumizi ya wahusika katika riwaya za kimajaribio yamekuwa ya kipekee zaidi,

kiasi cha kuzifanya riwaya hizo kujenge maana fiche. Makala hii, imebaini kuwa riwaya hizi zimetumia wahusika wenye kubeba umajaribio wa hali ya juu na hivyo kuwa na maana fiche ndani yake. Wahusika hao huweza kugawiwa katika makundi mbalimbali kulingana na sifa zinazotumika kusawiriwa kwao, kama vile; Wahusika jumui, wahusika wa kidhanaishi, wahusika wa kiitikadi, wahusika kinyonga, wahusika wa kisasili, wahusika wa kinjozi, wahusika wa kiishara na wahusika wa kimwingilianomatini (Mohamed, 1995; Madumulla, 2009; Njogu na Chimerah, 2011 pamoja na Wamitila 2015). Mgawanyo huu, umetumika katika makala haya na kubaini kuwa yapo makundi yaliyotumika katika riwaya husika. Kila kundi limekuwa na dhima maalum katika riwaya zake. Dhima zote hizo zikiwa na lengo la kujenga maana fiche katika riwaya husika.

### 1.4 Nadharia na Mbinu za Ukushanyaji na Uchambuzi wa Data

Kuna nadharia mbalimbali zinazoweza kutumika kuchambua maana katika kazi za kifasihi kama vile Uhakiki Mpya, Mawasiliano, Semiotiki na kadhalika (Olsen, 1982). Katika makala haya tumeongozwa na nadharia ya Semiotiki. Neno "semiotiki" lina asili ya Kiyunani "*semeion*" ambalo humaanisha ishara na linatumiwa kueleza mielekeo na makundi fulani ya kihakiki. Kihistoria, nadharia hii iliibuka miaka ya 1970 kipindi ambacho kulikuwa na mwelekeo mkubwa wa kuiendeleza zaidi Nadharia ya Umuundo ambao ulikuwa umetawala katika uchambuzi wa kazi za kifasihi miaka ya 1960. Nadharia hii iliasisiwa na mwanaisimu miundo Ferdinand de Saussure (1916) na Mwanafalsafa wa Kimarekani Charles Sanders Pierce (1931). Aidha, nadharia hii iliendelezwa na wataalamu mbalimbali kama vile Roman Jacobson, Valentin Voloshinov, Mikhail Bakhtin, Jacques Derrida, Umberto Eco, Tzvetan Todorov, Julia Kristeva na Roland Barthes (Selden, 1985).

De Saussure (1961) anaitazama nadharia hii katika mkabala wa kisayansi unaojishughulisha na uchunguzi wa mifumo ya ishara mbalimbali. Mtaalamu huyu anaeleza kuwa kilicho cha msingi katika nadharia hii ni uhusiano baina ya kitaja na kitajwa ili kuweza kupata maana ya ishara husika (Chandler, 2007)**.** Kutokana na ufafanuzi huu, tumebaini kuwa maana ya kitu inapatikana kwa kuangalia uhusiano uliopo baina ya kitaja (kiwakilishi) na kitajwa (kinachowakilishwa). Nadharia hii imegawiwa katika misimbo mitano mikuu kama msingi wa uchambuzi wa ishara katika matini. Barthes anaifafanua misimbo hiyo kuwa ni msimbo wa kiishara, kimatukio, kiurejelezi, kiseme na kihemenitiki. Makala hii imetumia msimbo wa kiishara ili kufikia lengo lake. Hivyo, msimbo wa kiishara umetumika kuchambua ishara zilizotumika katika riwaya teule ili kuibua maana zake fiche.

Utafiti wetu ulifanyika maktaba na ulihusisha riwaya ya Nagona. Riwaya hii iliteuliwa kwa kutumia mbinu ya usampulishaji lengwa. Mbinu hii, iliteuliwa kwa sababu mtafiti alilenga kundi mahsusi la riwaya, kundi ambalo lina sifa ya kuwa ni riwaya za kimajaribio. Riwaya zilizo katika mkondo huu ni chache, hasa katika fasihi ya Kiswahili. Kwa hivyo kutokana na lengo letu ikiwa pamoja na vitafitiwa kuwa na sifa za kipekee, usampulishaji lengwa ulikuwa ni muwafaka zaidi. Aidha, data katika riwaya teule zikusanywa kwa njia ya usomaji matini. Njia hii ilitupa fursa ya kuingia katika matini ya riwaya ya *Nagona* ili kubaini usawiri wa wahusika na ujenzi wa maana fiche. Data zilizopatikana zilichanganuliwa kwa kutumia mkabala wa kitaamuli ambapo hoja kuhusu wahusika na mchango wao katika ujenzi wa maana zilitolewa maelezo ili kutimiza malengo ya makala haya.

## 2.0 Wahusika wa *Nagona* katika Ujenzi Wa Maana Fiche

Usawiri wa wahusika na uhusika wao katika riwaya ya *Nagona* unaonesha kuwa, wahusika ni kipengele cha kisanaa ambacho kimetumika kujenga maana fiche katika riwaya. *Nagona* imetumia kipengele hiki kipekee kiasi cha kuwa tofauti na usawiri wa wahusika katika riwaya za mikondo mingine. Makala hii imewagawa wahusika katika makundi matatu makuu. Makundi hayo ni wahusika wa kiitikadi, wahusika jumui na wahusika wa kisasili. Uchambuzi wa wahusika umeongozwa na misingi ya Nadharia ya Semiotiki; kupitia msimbo wa kiseme. Msimbo huu unajikita zaidi katika kuangalia namna wahusika wanavyojengwa katika hadithi kwa kuangalia lugha, uhusiano pamoja na matendo yao katika kuipa maana kazi ya fasihi. Wahusika hao ndio wanaojenga matukio, ishara na hata kudokeza mambo yanayohitaji urejelezi wa aina fulani katika jamii. Khamis (2007b) anaeleza kuwa, wahusika wa kimajaribio hawana tabia pambanuzi wala tabia za kimaumbile za kibinadamu bali ni wahusika ambao wapo kiishara zaidi. Faustine (2018) anashadidia hoja hiyo kwa kusema kuwa, kazi hizi za kimajaribio zimekuwa na ukiushi wa kaida za kijadi za uandishi katika usawiri wa wahusika na uhusika wao. Kutoakana na upekee huo, usawiri umefanya wahusika hawa kuwa ni ishara ambazo zinajenga maana fiche. Wamitila (1999) anaeleza kuwa; majina, tabia na matendo ya wahusika yana jukumu katika usomaji wa kazi ya fasihi kupata maana ya ziada ya kazi hiyo. Hivyo, wahusika ni kipengele cha kisanaa ambacho kimetumika kama kijenzi cha maana fiche katika riwaya teule.

Jedwali lifuatalo linaonesha muhtasari wa data kuhusu wahusika wa kiitikadi katika riwaya ya *Nagona*. Jedwali limefafanua kundi la wahusika, matendo yao, umajumui wa mhusika na maana fiche zinazojitokeza, pamoja na uhusiano wa kisemiotiki kati ya viashirii na viashiriwa vilivyobainishwa kupitia uchambuzi wa data.

**Jedwali Na. 1: Wahusika Walivyotumika Kama Mbinu ya Kisanaa Katika Kujenga Maana Fiche katika Riwaya ya Nagona**

| Kundi la Wahusika | Matendo ya Wahusika | Itikadi za Mhusika / Maana Fiche | Viashirii na Viashiriwa |
|---|---|---|---|
| Nabii na Mtume (Itikadi ya Kidini) | Kusambaza "neno"; kufasiri maandiko; kupokea upinzani na kukashifiwa; kushirikiana na wafuasi katika kusambaza ujumbe wa kiimani. | Wawakilishi wa kundi lenye mamlaka ya kiroho na imani ya kidini, likisimama kinyume na falsafa za kifalsafa za Magharibi. Wanaunganisha nafasi ya mwalimu wa kiroho na mfasiri wa maandiko matakatifu. | **Viashirii**: Majina na istilahi zenye asili ya kidini, Mfano: "neno", "njia", "nukta".<br>**Viashiriwa**: Uongozi wa kiimani, mamlaka ya kiroho, na uhusiano na matukio ya kihistoria ya dini. Mgongano wa kidini dhidi ya falsafa za Magharibi. |
| Plato, Socrates, Aristotle, Hegel, Darwin, Marx, Freud (Itikadi ya Kifalsafa) | Kufikiria kwa kina; kuhoji njia; kusawiriwa wakiwa wamefungwa vitambaa machoni; kuweka vikwazo katika "njia" ya kweli. | Wawakilishi wa fikra za kifalsafa na mitazamo ya kisayansi inayotofautiana na misingi ya kiimani ya kidini. Wanawakilisha akili za ki-Magharibi zinazojitegemea katika tafsiri ya maisha na imani. | **Viashirii**: Majina ya kifalsafa, vitendo vya kufikiri na kuhoji, taswira ya kufungwa macho.<br>**Viashiriwa**: Upofu wa kiimani, changamoto za fikra huru dhidi ya imani ya dini, na tafsiri ya maisha inayopingana na mafundisho ya kiroho. |
| **Mimi (Mhusika wa Kimajumui)** | Kufungua viwanda katika nchi nyingi; kulima mashamba; kuchimba madini; kutawala uchumi wa dunia; kutengeneza silaha; kusaidia serikali; kukopesha maskini; kushika nafasi za Rais, Daktari, Sheikh, Mhandisi, Profesa. | Ishara ya nguvu zinazokandamiza tabaka la chini. | 1. Mhusika kama ishara – Nafasi na mamlaka anazobeba ni kiashirii cha nguvu zisizo na kikomo.<br>2. Ujumlishaji wa nafsi nyingi – "Wengi katika mmoja" huashiria muunganiko wa mamlaka.<br>3. Mabadiliko ya nafsi – Kutoka kiongozi wa kisiasa hadi wa kiroho na kitaalamu.<br>4. Kisemiotiki: nafasi, majina, vitendo vya wahusika vinaashiria nguvu za kijamii na udhibiti wa kiuchumi. |
| **Paa (Mhusika wa Kifasihi Simulizi)** | Kucheza bao kwa ustadi; kusawiriwa kama mnyama (paa), mwanamke mrembo, na ndege; kutoa mwanga wa ajabu; kuruka mlima; kuacha kitambaa chenye maandishi ya dhahabu. | Anabeba sura na uwezo wa viumbe mbalimbali visivyo vya kawaida, akiwakilisha maarifa, ukweli, na utakatifu; ishara ya kiumbe au mji wenye hadhi na anayetarajiwa na kila mtu. | **Viashirii:** mabadiliko ya umbo (mnyama, mwanamke, ndege), mwanga wa ajabu, kitambaa cha dhahabu, ustadi wa bao.<br>**Viashiriwa:** uwezo wa kipekee wa kiroho/kiakili, heshima na hadhi ya juu, ishara ya hekima na ukweli. Mabadiliko ya umbo huashiria uwepo katika nyanja tofauti za uhalisia na kiroho. |

Data iliyooneshwa katika Jedwali Na. 1 hapo juu imemwongoza mtafiti kuchambua matumizi ya wahusika wa kiitikadi kama mojawapo ya mbinu za kisanaa zilizotumika kujenga maana fiche katika riwaya teule. Kwa kuzingatia misingi ya Nadharia ya Semiotiki, imebainishwa jinsi majina, matendo na nafasi za wahusika waliotajwa kwenye jedwali hilo yalivyotumika kama ishara zenye kujenga na kuibua maana za ndani. Maana hizo fiche zimebeba mitazamo ya kidini, kifalsafa, kisiasa na kitamaduni, na zimekuwa nyenzo muhimu katika kuendeleza dhamira kuu za kazi husika. Uchambuzi unaofuata unajadili kwa kina masuala haya kwa kila riwaya.

## 2.1 Mhusika wa Kiitikadi

Mhusika wa kiitikadi ni mhusika anayewakilisha imani, falsafa au matabaka yaliyobayana ili kuyabainisha mawazo makuu yanayofumbata kazi yenyewe, (Mohamed, 1995; Wamitila, 2015 na Kawira na Kisurulia, 2017). Mwandishi wa kazi ya fasihi husawiri wahusika katika hali ya kuwabebesha mawazo fulani ambayo ni msingi wa mwelekeo wa kiutamaduni, kiuchumi au kisiasa kulingana na jamii husika. Kazi hii imebaini kuwa, riwaya teule zimetumia mhusika wa kiitikadi kama kijenzi cha maana fiche katika kazi hizo. Huenda maana zinazodokezwa zinahusiana na itikadi fulani. Itikadi ambayo huweza kuwa nzuri au mbaya kulingana na tabaka au jamii fulani. Data zetu zinaonesha kuwa wahusika wa kiitikadi wametumiwa

katika riwaya ya *Nagona* kwa kupitia wahusika Nabii na Mtume, pia kuna kundi la akina Plato, Socrates, Aristotle, Hegel, Darwin, Marx, Frend. Wahusika hawa wamekuwa ni ishara na kudokeza maana za kiitikadi katika mielekeo mbalimbali.

Riwaya ya *Nagona* imetumia wahusika wa kiitikadi katika makundi mawili tofauti. Kuna kundi la viongozi wa dini na kundi la wanazuoni wa kifalsafa. Ukifuatilia matukio yao, yanajenga ishara fulani ambayo yanajenga ufiche wa maana ndani yake. Wahusika Nabii na Mtume ni viongozi wa dini zinazotokana na Ibrahim. Wahusika hawa wamechorwa wakiwa na sifa ya kihistoria na umwingiliano matini katika vitabu vya dini ya Uislamu na Ukristo kwa kurejelea moja kwa moja kwa Mtume Muhamad na Yesu Kristo (Nabii Issa). Kauli na matendo ya wahusika hawa yamekuwa ni ishara zinazobeba maana ambazo haziko wazi moja kwa moja. Kama data yetu inavyothibitisha kwa kusema:

> Halafu Nabii alikohoa kidogo kusafisha koo tayari kuzungumza. … Niliweka nukta baada ya neno la mwisho wa sura. … Walinifikiria kichaa, wale ambao hawakuniamini. … Walioteuliwa walijitahidi walivyoweza kuweka katika kumbukumbu niliyoyasema. Tatizo ni fasili na ufafanuzi. … Waliniua mimi badala ya kuua *Sphinx*”
>
> Mtume naye alianza: “Yote yaliyosemwa yalikuwa wazi na wafuasi wangu waliyasikia. Walikuwa wenzangu. Baadhi yao waliyasikia nikiyakariri mbele ya Gabrieli na waliyajua vyema wakayaweka katika maandishi. … Tatizo bado ni fasili. Palitokea ashab, tabilina na tafsiri. … Mimi pia niliweka nukta baada ya neno la mwisho wa sura.”
>
> **Chanzo**; Kezilahabi (2011: 46 – 47)

Data hii inaeleza wahusika Nabii na Mtume wanavyosimulia matukio yaliyowafika. Wahusika hawa wamekuwa wakitoa ishara na kuonesha kuwa kuna ufiche wa maana ndani yake. Mazungumzo yao, yamedokeza njia au mwongozo ilivyowekwa wazi. Njia na mwongozo ni viashirii vinavyobeba ufiche wa maana unaowahusu wahusika hawa. Nabii anaeleza kuwa wapo waliomkataa na kusema si nabii na kumuita kichaa. Pia, wapo waliomuamini kuwa ni nabii wa kweli aliyeletwa kumkomboa binadamu. Nabii anaelezea juu ya wafuasi wake walivyojitahidi kunukuu kwa usahihi kile walichokipata kutoka kwake. Shida ya neno (maandiko) ikajitokeza kutoka kwa wafasiri na wachambuzi waliokuja baadaye kufasiri na kuchambua andiko hilo. Neno nalo ni kiisharii kinachobeba maana fiche kwa mhusika huyu. Viashirii vya lugha na matukio waliyopewa wahusika hawa vinajenga ishara zinazobeba maana fiche inayoweza kufahamika kupitia viashiriwa vyake. Maelezo haya, yanaonesha kuwa, kuna maana fiche kutokana majina na matendo ya wahusika hao.

Kwa upande wa Mtume, data inaeleza alivyopewa neno na kuwekwa katika maandishi. Usawiri wa mhusika Mtume akiambatanishwa na ashab, tabilin na tafsiri ni viashirii vinavyobeba viashiriwa vivyonajenga maana fiche juu ya mhusika Mtume. Pia, mhusika Mtume anasawiriwa akieleza kuwa, aliweka nukta baada ya neno la mwisho wa sura. ‘Neno’ na baadaye maandishi ni viashirii vinavyodokeza mhusika Mtume ni nani katika ulimwengu halisi. Hii inadokeza maana fiche inayojitokeza katika riwaya hii kupitia mhusika huyu.

Kwa jumla, kinachojenga ufiche katika wahusika hawa, kwanza ni suala la kutumia majina haya ya Nabii na Mtume, majina yanayodokeza itikadi ya kidini. Pili, kutumia maneno kama vile ‘neno, njia na kichaa’ kumhusisha mhusika Nabii na Sphinx. Pia, kuwaweka pamoja wahusika ambao katika dunia wanaonekana kuwa katika zama mbili tofauti. Msimbo wa kiishara unatuongoza kusema kuwa, mtindo wa kuwatumia wahusika hawa unajenga ishara zizonabeba maana fiche inayofahamika kupitia viashiriwa vyake. Maana zinazodokezwa kupitia wahusika hawa ni kuwa, Nabii na Mtume walioelezewa katika vitabu vitakatifu kuwa ndugu na walikuja kutangaza neno moja juu ya kumuabudu Mungu wa aridhi na mbingu. Maelezo haya yanathibitishwa katika (Qur-ani 3:3) kwa kusema kuwa “Amekuteremshia kitabu kwa haki, kinachosadikisha yaliyo kuwa kabla yake. Na aliteremsha Taureti na Injia.” Hoja hii inaendana na mawazo ya Diegner (2005) na Malugu (2019) yanayoeleza kuwa, ili upate maana katika riwaya ya *Nagona* kuna haja ya kurejea katika matukio ya kidini, ambayo yanajitokeza zaidi katika Biblia na Kur-ani. Kwa jumla, wahusika hawa wametumika kujenga itikadi ya kidini ambayo imejengwa kwa fiche ndani ya riwaya hii.

Pia, wahusika Plato, Socrates, Aristotle, Hegel, Darwin, Marx, Frend na wengine ni wahusika wa itikadi ya kifalsafa. Utafiti umebaini kuwa, majina na matendo ya wahusika hawa yamekuwa na maana fiche ambazo zinadokeza masuala ya kiitikadi. Mfuatano wa matukio unaonekana kuwa itikadi zao ni tofauti na itikadi za Nabii na Mtume. Pia, inabainika kuwa, maana nyingine inayodokezwa na wahusika hawa ni udokezaji wa siasa ya kimataifa hasa katika masuala ya Uafrika na Umagharibi. Masuala haya yanajitokeza kupitia ishara zilizosawiriwa kupitia matendo ya wahusika hawa. Maelezo haya yanathibitishwa kupitia data Na. 4.2.1.1 (b) kama ifuatavyo: 4.2.1.1 (b)

> “Uwaonao katika duara hii ni kikundi kidogo tu cha waliokuwa wabishi katika usakaji wa njia. Yule pale ni Plato, na yule ni Socrates. Huyu hapa ni Aristotle. Yule ni Hegel, huyu Darwin na waliokaribiana nawe ni Marx na Freud, na huyu ni Nietzsche. Ilibidi wafungwe vitambaa machoni kwa sababu walikuwa karibu kukata tamaa. Njia niliiweka wazi, tena wazi kabisa, wima bila kupinda; ukungu wote niliuondoa. Hiki kikundi kidogo tu cha wale walioiwekea

njia miba, ngazi za kupandia na madaraja yasiyoaminika."
**Chanzo**: Kezilahabi (1990: 26)

Data hii inaonesha wahusika hawa wanavyotofautiana kiitikadi na wahusika Nabii na Mtume. Kwa mujibu wa data hii wahusika hawa wameoneshwa wapo kwenye duara wakiwa wamefungwa vitambaa kwa sababu walikuwa karibu kukata tamaa na rehema za Mungu. Walikata tamaa kwa matendo yao ya kuiwekea njia miiba, ngazi za kupandia na madaraja yasiyoaminika. Data hii imetumia maneno kama 'wabishi katika usakaji wa njia, miba, ngazi na madaraja' ni viashirii vinavyojenga ishara na kudokeza maana fiche katika data hiyo. Hoja hii inathibitishwa kupitia msimbo wa kiishara kwa kuonesha majina na matendo ya wahusika hao yalivyokuwa viashirii vinavyojenga viashiriwa vya maana. Viashirii hivyo, vinadokeza maana fiche ya kuwa, wahusika hawa wamekuwa hawafati njia sahihi iliyowekwa na Mungu. Hii inamaanisha kuwa, wahusika hawa wametumia muda na taaluma zao kuweka vikwanzo katika kufuata njia sahihi ilowekwa na Mungu wa Aridhi na Mbingu. Utafiti ulionesha kuwa, maana hii inatokana na namna walivyosawiriwa katika sifa na matendo yao katika kazi hii.

Kwa jumla, Wahusika kama Mtume na Nabii pamoja na Plato na Aristotle ni pande mbili zenye itikadi tofauti ambazo zinajenga maana fiche. Hoja hii inaenda sambamba na maelezo ya Mohamed (1995) kwa kusema kuwa, waandishi wa kimajaribio hutumia wahusika wenye uwezo mkubwa na kubeba itikadi tofauti zikiwemo za kifalsafa. Pia, Kavoi (2018) anasema kuwa, Kezilahabi ametumia wahusika kama Hegel, Marx, Plato kwa maana ya ndani zaidi ya ile ambayo unaweza kuipata.

### 2.2 Wahusika Jumui

Mhusika jumui ni mhusika anayesawiriwa kwa sifa na udhihirisho unaomfanya awakilishe uhusika wa wahusika tofauti kwa wakati mmoja (Wamitila, 2015). Kutokana na sifa hiyo, mhusika huyu huwa hana sifa bayana za utunafsi kama mhusika bali anadhihirishwa kiutendaji katika kazi au matini fulani ya kifasihi. Kazi hii imebaini kuwa mhusika wa aina hii, ametumika katika kazi teule kama ni kijenzi cha maana fiche kwa namna alivyojengwa kama ni ishara ambayo inabeba maana ya wazi na isiyo wazi. Data zetu zinaonesha kuwa mhusika jumui ametumika katika riwaya hii. Riwaya hii imetumia mhusika 'Mimi' kama ni mhusika jumui.

Riwaya ya *Nagona,* kuna matumizi ya mhusika 'Mimi'. Mhusika huyu ana sifa ya ujumui. Mwandishi anamsawiri kama ni mhusika anayebeba nafsi nyingi kwa wakati mmoja. Hali hiyo inatokana na ujumuishaji wa nafsi na majukumu ya wahusika tofauti kwa wakati mmoja, kama vile kuwa ni rais, padri, sheikh, daktari nakadhalika. Hali hii inajenga ishara na kujenga maana fiche. Maelezo haya yanathibitika kwa kupitia data ifuatayo:

"Niliweza kufungua viwanda katika nchi nyingi ulimwenguni. Nililimisha mashamba na nilichimba madini. Nikatawala uchumi wa dunia."
"Hizo pesa ulizitumiaje?"
...
"Kiasi nilitumia kutengenezea silaha kali kulinda usalama wangu, kiasi nilisaidia serikali na zingine niliwakopesha maskini."
...
"Kama kuna vichaa wengine kama wewe katika ulimwengu huu basi tumekuwa tukiendeshwa na wazimu."
"Nimesema tuko wengi katika mmoja."
...
"Rais!"
"Daktari!"
"Sheikh!"
"Mhandisi!"
"Profesa!"
**Chanzo**: Kezilahabi, (1990: 88 - 91)

Maelezo haya yanaeleza kuwa mhusika 'Mimi' anawakilisha watu wa tabaka la juu linalowakandimiza watu wengi wa chini. Ndio maana anathibitisha kuwa yeye ana nafasi ya kuwa Rais, Daktari, Sheikh, Mhandisi, Profesa na hata nafasi nyingine. Kusawiriwa juu ya nafasi hizi ni mbinu ya mwandishi kumjenga mhusika kama ni ishara. Ishara ambayo ina maana fiche ndani yake. Kwa mujibu wa msimbo wa kiishara, maelezo kama vile, 'kufungua viwanda katika nchi nyingi, kulimisha mashamba, kuchimba madini, kutawala uchumi, kutengeneza silaha, kusaidia serikali na kukopesha masikini pamoja na kuwa na nafasi za nafsi mbalimbali kama vile Urais, Udaktari' na nyinginezo ni viashirii vinavyodokeza maana fiche kwa mhusika Mimi.

Kwa jumla, wahusika jumui wametumiwa katika kazi teule wakiwa ni ishara zinazojenga maana fiche ndani yake. Ndio maana Maguju (2004) anaeleza kuwa riwaya hii imetumia wahusika wa kipekee kutokana na wahusika wake kutokuwa na maumbo maalum, kubadilika sura na kuwa na majukumu ya uhusika zaidi ya mmoja. Mambo ambayo yanatoa ishara tofauti na kujenga maana fiche. Pia, Khamis (2007a) anaeleza kuwa, *Nagona* imebeba ujumbe mzito kutokana na kutumia mhusika "Mimi", mhusika wa kipekee asiyekuwa na nafsi maalumu. Maelezo haya yanathibitisha kuwa, wahusika hawa hawakusawiriwa kwa bahati mbaya, bali ni kwa ajili ya kuwa ishara na vijenzi vya maana fiche. Wahusika wanaohitaji umahiri katika kuwasawiri na kutoa maana unayoihitaji, (Njogu na Chimerah, 2011).

### 2.3 Wahusika wa Kisasili

Wahusika wa kisasili ni wahusika wa kifasihi simulizi wenye sifa zinazowakweza juu ya wahusika wa

kawaida wanaopatikana katika mazingira yao. Wahusika wa aina hii huweza kuwa wanyama, wadudu, mimea, mashetani miungu na viumbe wengine, (Senkoro, 2011). Wahusika hawa, wanafanana na wahusika wa kwenye ngano. Ila wahusika wa kisasili huwa hawafi kwa njia ya kawaida, (Wamitila, 2015). Wahusika wenye sifa hiyo, wametumika katika riwaya ya *Nagon*a na kubainika kuwa ni sehemu ya kipengele cha kisanaa kilichotumika kujenga maana fiche katika kazi hiyo. Data zetu zinaonesha kuwa mhusika wa kisasili ametumika kupitia riwaya ya *Nagona* kwa kutumia mhusika 'Paa'.

Katika riwaya ya *Nagona* mhusika Paa amekuwa na sifa ya mhusika wa kisasili. Mhusika huyu amechorwa akiwa na wasifu wa viumbe tofauti, ukiwemo; mnyama aina ya Paa, mwanamke mrembo na hata ndege anayeweza kuruka. Usawiri wa mhusika huyu, unampa sifa ya kuwa ni mhusika wa kisasili. Hali hiyo inaonesha kuwa, mwandishi amemsawiri mhusika huyu ili kuwa ishara inayoweza kujenga maana fiche kwa wasomaji wake. Utafiti umebaini kuwa, mhusika huyu anabeba maana fiche kupitia jina, sifa, lugha na matendo yake kama ilivyooneshwa katika data ifuatayo:

> "Paa mnayemtaka, …anajua sana kucheza bao. Nataka acheze na mmoja kati yenu.
>
> …
>
> Nilimfunua paa kuanzia kichwani hadi miguuni. Alikuwa msichana mzuri ambaye hajapata kuonekana,
>
> …
>
> "Njia iko wazi! Wazi kabisa! …"Zima mshumaa" "Nitakuonaje" nilimwuliza. "Fikiri," alijibu. …Niliona mwili wake unaanza kutoa mwanga. … Nikiwa nimelala chini niliweza kumwona akiruka mlima halafu akatoweka machoni mwangu; kukawa na giza kibandani. "Aliacha kitambaa chake," …Katikati ya kitambaa hiki palikuwa pamenakishiwa kwa maandishi ya wino wa dhahabu neno "Nagona"
>
> **Chanzo**: Kezilahabi (1990: 59 - 69)

Maelezo haya yanaeleza mhusika Paa kuwa, hana utambulisho wa umbo mahususi. Mhusika huyu kuna wakati alisawiriwa kama mnyama. Kuna wakati amefafanuliwa kama ni mwanamke mrembo ambaye hajapata kuonekana. Kuna wakati amekuwa kama kitu chenye mwanga usiokuwa wa kawaida pamoja na kuwa na nguvu kama mpiganaji wa mieleka. Pia, kuna wakati alisawiriwa kama ndege. Sifa ambazo kwa hali ya kawaida haziwezi kukaa pamoja kwa kiumbe fulani kwa wakati mmoja. Sifa zote hizo zimekuwa ni viashirii vinavvyojenga maana fiche kupitia mhusika Paa. Kutokana na viashirii hivyo, mhusika Paa amesawiriwa kudokeza dhana ya elimu na ukweli katika jamii. Pia, Paa anadokeza utakatifu wa mtu au mji wenye hadhi na kutarajiwa na kila mtu katika dunia. Kwa jumla, maelezo haya yanatoa ishara ya Paa aliyesawiriwa kama mhusika wa kisasili na kijenzi cha maana fiche katika riwaya hii. Mhusika huyu amejitokeza katika sura na sifa za viumbe tofauti ikiwemo mnyama, msichana na ndege.

Wahusika ni kipengele cha kisanaa ambacho kimetumika kujenga maana fiche katika riwaya teule. Riwaya hizi zimetumia kipengele hiki kipekee kiasi cha kuwa tofauti na usawiri wa wahusika katika riwaya za mikondo mingine. Utafiti ulibaini kuwa, wahusika wa riwaya hizi wamekuwa wa aina tatu kuu. Wahusika jumui, wahusika wa kiitikadi na wahusika wa kivisasili. Kama ambavyo Khamis (2007b) anaeleza kuwa, wahusika wa kimajaribio hawana tabia pambanuzi wala tabia za kimaumbile za kibinadamu bali ni wahusika ambao wapo kiishara zaidi. Faustine (2018) anashadidia hoja hiyo kwa kusema kuwa, kazi za kimajaribio zimekuwa na ukiushi wa kaida za kijadi za uandishi katika usawiri wa wahusika na uhusika wao. Kutokana na upekee huo usawiri umefanya wahusika hawa kuwa ni ishara zizonajenga maana fiche. Hivyo, wahusika ni kipengele cha kisanaa ambacho kimetumika kama kijenzi cha maana fiche katika riwaya teule.

## 3.0 HITIMISHO

Wahusika ni kipengele cha kisanaa ambacho kimetumika kujenga maana fiche katika riwaya ya kimajaribio. Riwaya hii imetumia kipengele hiki kipekee kiasi cha kuwa tofauti na usawiri wa wahusika katika riwaya za kawaida. Makala imebaini kuwa, wahusika wa riwaya ya kimajaribio wamekuwa na aina kuu tatu za uhusika. Wahusika jumui, wahusika wa kiitikadi na wahusika wa kisasili. Wahusika hawa wamekuwa na sifa kubwa ya udhanaishi, kama walivyoeleza Njogu na Chimarah (2011) kwa kusema kuwa Kezilahabi amejikita sana katika kazi zenye sifa za udhanaishi. Wahusika hawa wametumika kudokeza maana mbalimbali zikiwemo; usaliti katika imani za kidini na elimu ya falsafa kuwa ni kikwanzo katika imani za kidini. Kudokeza suala la ukoloni na ukoloni mamboleo pamoja na suala la ukweli na utukufu wa miji katika dunia. Maana hizi zimehusishwa na vitabu vya kidini kwa sababu, Biblia, Kur'ani na baadhi ya vitabu vingine vya dini na maadili ni sehemu kuu ya fasihi, (Njogu na Chimerah, 2011). Hii inatokana na kuwa, kuna uhusiano mkubwa kati ya maandishi ya kidini na kazi ya fasihi, (Osore, 2018). Ndio sababu, maana nyingi zilizojitokeza zimejikita zaidi katika masuala ya kidini na kuziegemeza katika ushahidi wa vitabu vitakatifu vya kidini. Kutokana na matokeo hayo, makala haya yanapendekeza kuwa, kuna haja ya kutafiti uhusiano wa maandiko ya kidini na riwaya za kimajaribio hususani riwaya za Kezilahabi. Kutafiti mitindo ya usawiri wa wahusika katika riwaya za kimajaribio za Kezilahabi. Kadhalika, kulinganisha usawiri wa riwaya za kimajaribio kwa kuangalia riwaya za Kezilahabi na riwaya za waandishi wengine wa kimajaribio.

## 4.0 MAREJELEO


- Al-Barwani, A. M. (2017) Tarjama ya "Al-Muntahab" katika Tafsiri ya Qur-ani Tukufu ya Kiswahili. Mascat: Hakuna Mchapishaji.

- Diegner, L. (2005) "Intertextuality in the Contemporary Swahili Novel: Euphrase Kezilahabi's *Nagona* and William E. Mkufya's *Ziraili na Zirani*". *Swahili Forum*, Na. 12: 25 – 35.
- Faustine, S. (2018) "Dhima ya Mtindo wa Uhalisiajabu katika Riwaya ya Kiswahili: Uchambuzi wa Babu Alipofufuka". Katika M. S. Khatibu, H. Kh. Juma na K. O. Makame (wah.) *JAHAZI.* Zanzibar: Baraza la Kiswahili la Zanzibar. kur. 23 – 37.
- Jilala, H. (2016) *Msingi ya Fasihi Linganishi; Nadharia, Mbinu na Matumizi*. Dar es Salaam: Daud Publishing Company.
- Kawira, S. na Kisurulia, S. (2017) "Wahusika, Uhusika na Mtazamo katika Riwaya ya Kiswahili". *MULIKA 2017 Toleo Maalum*: *Makala ya Kongamano la CHAUKIDU 2016*. Dar es Salaam: TATAKI. kur. 119 – 132.
- Kezilahabi, E. (2011) *Nagona*. Nairobi: Vide-Muwa.
- Khamis, S. A. M. (2005) "Signs of New Features in the Swahili Novel". Research in African Literature, Spring, V. 26 (1): 91 – 108.
- Khamis, S. A. M. (2007a) "Vionjo vya Riwaya Mpya ya Kiswahili". *Kioo cha Lugha*, Na. 5: 13 – 23.
- Khamis, S. A. M. (2007b) "The Swahili Novelist at the Crossroad: The Dilemma of Identity and Fecundity". *Swahili Forum*, Na. 14: 165 – 180.
- Madumulla, J. S. (2009) *Riwaya ya Kiswahili: Nadharia, Historia na Misingi ya Uchambuzi*. Dar es Salaam: Mture Educational Publishers Limited.
- Magaju, J. K. (2004) Uhalisiajabu katika Riwaya ya *Babu Alipofufuka* (2001) ya S. A. Mohamed na *Bin-Adamu* (2002) ya K. W. Wamitila. Tasnifu ya Shahada ya Uzamili (Haijachapwa). Chuo Kikuu cha Kinyata, Nairobi.
- Malugu, A. (2019) "Matumizi ya Jazanda katika Tamthiliya ya *Kaptula la Marx*". *JAHAZI*, Toleo Na. 3: 241 – 254.
- Martin, W. (1986) Recent Theories of Narrative. Cornell University Press, New York.
- Mbatiah, M. (1998) "Mienendo Mipya katika Uandishi wa Kezilahabi: *Nagona* na *Mzingile*". *Mulika*, Na. 24: 1 – 24.
- Mbatiah, M. (2019) "Maendeleo ya Bunilizi ya Kimajaribio katika Kiswahili". Katika A. S. Ponera na Z. A. Badru (wah.) *Koja la Taaluma za Insia.* Dar es Salaam: Karljamer Publishers Limited. kur. 78 – 104.
- Mkufya, W. (2005) "Mazungumzo na Lutz Diegner juu ya Riwaya ya Zirail na Zirani". *Swahili Forum*, Na. 12: 37 – 62.
- Mohamed, S. A. (1995). *Kunga za Nadhari ya Kiswahili: Riwaya, Tamthilia na Hadithi Fupi*. Nairobi: East African Educational Publishers, Ltd.
- Mwamzandi, I. (2013) "Riwaya Teule za Karne ya Ishirini na Moja na Udurusu wa Nadharia za Fasihi". *Swahili Forum*, Na. 20: 48 – 66.
- Njogu, K. na Chimera, R. (2011) *Ufundishaji wa Fasihi; Nadharia na Mbinu*. Nairobi: Jomo Kenyatta Foundation.
- Olsen, S. H. (1982) "The "Meaning" of Literary work." Katika Autumn (mh.) New Literature History. The John Hepkeins University Press. Kur. 13 – 32. Kutoka https://www.jostor.org/stable/468955 imesomwa tarehe 5/2/2020 saa 4:09 PM.
- Osore, M. (2018) "Fasihi Andishi ya Kiswahili na Swala la Dini: Mifano ya Riwaya za Said Ahmed Mohamed na za Euphrase Kezilahabi". Katika Kandagor na Mukuthuria (wah.) *Fasihi ya Kiswahili: Utafiti na Maendeleo yake*. CHAKAMA. Kur. 188 – 199.
- Pembe, H. (2017) "Majina ya Wahusika katika Fasihi ya Kiswahili". *MULIKA 2017 Toleo Maalum*: *Makala ya Kongamano la CHAUKIDU 2016*. Dar es Salaam: TATAKI. kur. 98 – 118.
- Ponera, A. S. & Mkomwa, S. (2019) "Utanzuaji wa Vibandiko Kama Mkakati wa Kuzielewa Riwaya za Kifalsafa: Mfano wa Riwaya ya *Nagona"*. Katika Ponera & Badru (wah.) *Koja la Taaluma za Insia*. Dar es Salaam: Karljamer Publisher limited. kur. 459 – 480.
- Samwel, M. (2015) *Umahiri katika Fasihi ya Kiswahili: Mwongozo kwa Mwanafunzi na Mwalimu wa Fasihi Simulizi na Andishi*. Dar es Salaam: Mevel Publishers (MVP).
- Senkoro, (2011) *Fasihi*. Dar es Salaam: KAUTTU Limited.
- The Gideons International (2015) *Kitabu cha Agano Jipya la Bwana na Mwokozi Wetu Yesu Kristo*. Nashville: National Publishing Company.
- Wamitila, K. W. (1999) "What's in a Name Towords Literary ONOMASTIC in Kiswahili Literature". *Mulika*. AAP. 60: 35 – 44.
- Wamitila, K. W. (2003) *Kamusi ya Fasihi: Istilahi na Nadharia*. Nairobi: Focus Publications Ltd.
- Wamitila, K. W. (2015) *Kanzi ya Fasihi 1: Misingi ya Uchanganuzi wa Fasihi*. Nairobi: Vide-Muwa Publishers Ltd.


**Cite This Article:** Gora A. Haji, Ernesta S. Mosha, Ramadhani T. Kadallah (2026). Wahusika wa Riwaya za Kimajaribio: Uchunguzi wa Maana Fiche Katika Riwaya ya *Nagona*. *East African Scholars J Edu Humanit Lit, 9*(8), 445-452.